

# MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA



## TAARIFA KWA UMMA

29 Juni, 2018

### UPOTOSHAJI KUHUSU USALAMA WA DAWA YA PANADOL

1. Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ni wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto yenye jukumu la kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi nchini.
2. Kwa lengo la kujiridhisha kuwa dawa zilizopo nchini zinakidhi usalama, ubora na ufanisi, Mamlaka imeweka mifumo mbalimbali ya udhibiti ikiwa ni pamoja na mifumo ya tathmini na usajili, ukaguzi, uchunguzi wa kimaabara, ufuatiliaji wa usalama na ubora wa dawa kwenye soko.
3. Hivi karibuni kumekuwepo na video inayosambazwa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu usalama wa dawa aina ya **paracetamol** yenye jina la kibiashara la **Panadol** (iliyo katika muundo wa kidonge) kuwa inapomwagiwa maji inageuka kuwa kitambaa.
4. Kufuatia taarifa hiyo, TFDA inapenda kutoa ufafanuzi kuwa **taarifa hiyo si sahihi na kwamba dawa ya panadol ni salama kwa matumizi kama zilivyo dawa nyingine**. Aidha, bidhaa inayohusishwa na dawa tajwa ni kitambaa (tab towel) ambacho kimetengenezwa kwa muundo wa kidonge na juu hakuna lebo ya *Panadol* wala *paracetamol* kama inavyoelezwa na katika video inayosambazwa. Bidhaa hii hutumika zaidi katika mahoteli au maeneo mengine.
5. Kufuatia uvumi huo Mamlaka imefanikiwa kumpata mtu anayejiita Bw. Prince Elia Emmanuel Mhina, msambazaji wa video hiyo ambaye bado anaendelea kuhojiwa juu ya adhama yake ya upotoshaji wa wazi kuhusiana na bidhaa ya dawa.

6. Mamlaka inawahakikishia wananchi kwamba kupitia mifumo iliyopo itaendelea kufuatilia usalama wa dawa hiyo kwenye soko ili kuhakikisha kuwa dawa hiyo inaendelea kuwa salama kwa watumiaji.
7. Aidha, TFDA inatoa wito kwa mtu yeyote mwenye taarifa juu ya uwepo katika soko la Tanzania wa bidhaa inayolalamikiwa kutoa taarifa ofisi za TFDA Makao Makuu na ofisi za Kanda zilizopo Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya, Dodoma, Mtwara na Tabora au kupitia barua pepe ya [info@tfda.go.tz](mailto:info@tfda.go.tz), simu bila malipo 0800110084 au ofisi za afya za Halmashauri.
8. Rai inatolewa kwa wananchi kuepuka kusambaza taarifa zisizohakikiwa na TFDA kupitia mitandao ya kijamii ili kuondoa hofu na taharuki zisizo za lazima na kuendelea kushirikiana na TFDA katika kutoa taarifa pindi wanapokuwa na mashaka juu ya usalama na ubora wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kwa wakati.

**Agnes Sitta Kijo**  
**Kaimu Mkurugenzi Mkuu,**  
**Mamlaka ya Chakula na Dawa,**  
**S.L.P 77150,**  
**Dar es Salaam.**